

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI INATANGAZA  
NAFASI ZA MASOMO ZILIZOTOLEWA NA SERIKALI YA  
MAURITIUS, NGAZI YA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA  
MASOMO 2017-18**

**1 Sifa za muombaji**

- Asiyezidi miaka 25
- Awe amemaliza kidato cha sita na amefaulu daraja la kwanza au la pili au amehitimu ngazi ya Diploma.

**2 Utaratibu wa malipo**

Waombaji watakao bahatika kupata nafasi hizo watapatiwa malipo yafuatayo;

- i. Posho la kila mwezi Rs 8,300 kwa USD 266
- ii. Ada ya masomo Rs 100,000 kwa USD 3205 kwa mwaka
- iii. Tiketi kwa kipindi chote cha masomo hadi kumaliza.

**3 Njia za kufanya maombi**

Waombaji wote wanatakiwa waombe barua ya kujiunga na chuo (Admission Letter) kupitia mitandao ya vyuo vya Mauritius kama vifuatavyo;

<b>CHUO</b>	<b>ANUANI</b>
University of Mauritius	<a href="http://www uom ac mu">www uom ac mu</a>
University of Technology, Mauritius	<a href="http://www utm ac mu">www utm ac mu</a>
Universities des Mascareignes	<a href="http://www udm ac mu">www udm ac mu</a>
Fashion & Design Institute	<a href="http://www fdi ac mu">www fdi ac mu</a>

Mauritius Institute of Education	<a href="http://www.mie.ac.mu">www.mie.ac.mu</a>
Mahatma Gandhi Institute	<a href="http://www.mgirti.ac.mu">www.mgirti.ac.mu</a>
Rabindranath Tagore Institute	<a href="http://www.mgirti.ac.mu">www.mgirti.ac.mu</a>

Fomu ya maombi na maelekezo yake inapatikana katika mtandao ufuatao;

[http://ministry-education.govmu.org/English/Scholarships/  
Pages/default.aspx](http://ministry-education.govmu.org/English/Scholarships/Pages/default.aspx)

#### **4. Utaratibu wa kuwasilisha maombi**

Waombaji wa nafasi hizo watatakiwa kuwasilisha viambatisho vifuatavyo katika maombi yao;

- 1 Cheti cha kuzaliwa
- 2 Vivuli vyta Vyti vyta kumalizia masomo vyta "O" na "A" Level
- 3 Fomu ya Afya (Medical Report)
- 4 Kivuli cha pasi ya kusafiria
- 5 Nyaraka zote zinahusiana na masomo anayotaka kusomea

Kwa maelezo zaidi Kuhusiana na nafasi hizo fika;

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali – Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu chumba No.57.**